**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**


**SHULE YA SEKONDARI KAZIMA**

**S.L.P 369**


**Tarehe 21/11/2025**


**Namba za Simu**

| | |
|---|---|
| **Mkuu wa Shule** | **0786635179** |
| | **0762240716** |
| **M/Mkuu wa Shule** | **0713377442** |
| **Matron** | **0759760768** |


**KUMB NA ______________________________**

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI ____________________________________**

**S.L.P ____________________________________________________________**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAZIMA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA MKOA WA TABORA MWAKA 2026**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza katika Shule hii mwaka 2026

**2.** Shule ya Sekondari KAZIMA ipo umbali wa Kilometa 1.5 Mashariki mwa Mji wa Tabora Usafiri kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Tabora Nauli ni Shilingi 1000/= kwa pikipiki ni Shilingi 2000/= kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 13/01/2026, Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 10/01/2026

Mara upatapo barua hii na kuisoma kwa makini tafadhali unatakiwa kumpatia mwanaomahitaji yote stahili (yailyo orodheshwa). Ili kumwezesha afike shuleni mapema bila kupoteza muda wa masomo.

### 3. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

#### 3.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi (2) ndefu mpaka kifundo cha mguu, rangi ya damu ya mzee marinda boksi mbele na nyuma na marinda ya kawaida pembeni na mashati meupe(2) ya mikono mifupi.

ii. Rangi ya Hijab (juba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

iii. Sare ya Michezo ni sketi fupi ya solo na truck suit damu ya mzee yenye mistari mieupe pembeni, kwenye kola na mikononi isiyo na kofia,Uwanjani wanavaa Jezi za rangi ya damu ya mzee yenye mistari mieupe pembeni kama anacheza mchezo wa mpira wa miguu..

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi jozi mbili.

   (i) Soksi jozi mbili nyeupe.

   (ii) Sweta la damu ya mzee;

v. Nguo za kushindia gauni (2) za damu ya mzee, mshono wa solo. Kwa wanafunzi wa kiislam, nusu kanzu ya damu ya mzee na hijabu (juba) ya damu ya mzee inayofunika kifua

vi. Tisheti (T-shirt) 2 damu ya mzee zenye kola nyeupe na mstari mweupe.

vii. Tai ya damu ya mzee kitambaa cha suti.

**N.B: IWAPO MZAZI/MLEZI ATASHINDWA KUSHONA AU KUPATA SARE YA MWANAFUNZI KWA SABABU YOYOTE ILE, MZAZI ANAWEZA KUMSHONEA SARE HIZO KWA FUNDI WA NGUO ANAYEPATIKANA SHULENI KWA GHARAMA ZIFUATAZO;**

(i) Sketi 1 ya rangi ya damu ya mzee – Shs. 25,000/=

(ii) Gauni 1 ya kitambaa cha suti rangi damu ya mzee – Shs. 28,000/=

(iii) Mashati 1 nyeupe ya tomato ya mikono mifupi – Shs 7,000/=

(iv) Sweta la shule rangi damu ya mzee – Shs. 15,000/=

(v) T – Shirt ya rangi ya damu ya mzee yenye kola nyeupe na ufito wa damu ya mzee – Shs. 12,000/=

(vi) Truck suit za damu ya mzee zenye mistari myeupe pembeni na kola nyeupe yenye ufito wa damu ya mzee isiyo na kofia – Shs. 22,000/=

(vii) Sketi fupi ya michezo kwa wasichana – Shs. 20,000/=
(viii) Juba 1 nyeupe ya darasani Tshs. 14,000/=
(ix) Juba 1 damu ya mzee ya kushindia Tshs. 14,000/=
(x) Tai ya damu ya mzee kitambaa cha suti Tshs. 3,000/=
(xi) Jezi za mpira wa miguu Tshs. 12,000/=

**3.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari makubwa 15 kwa ajili ya masomo.(counter book quire 2)
ii. **Bima ya afya au Tsh 50,400. kwa jili ya matibabu ya mwanafunzi**
iii. Vitabu vya masomo yote kama kuna uwezekano.
iv. Dictionary ya ENGLISH – KISWAHILI.
v. Sanduku la chuma la kuhifadhia vitu vyake.
vi. Godoro moja inchi $2\frac{1}{2}$ kwa nne au sita.(Godoro imara)
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket la kijivu kwa anayehitaji, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe*;*
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.

**N.B Endapo mzazi atashindwa kupata vifaa kama ndoo, madaftari makubwa (counter book) na mashuka, vinapatikana dukani karibu na shule.**

**4. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na **Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**4.1 Sheria na Kanuni za Shule**

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
(iii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa/utakazopangiwa;
(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
(vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
(ix) Kutunza mali za shule;
(x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
(xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**4.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele; wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Kutokuwepo shuleni baada ya saa kumi na mbili(12:00) jioni.
ix. Uasherati,ushoga na mahusiano ya jinsia moja na kuolewa;
x. Kuwa mjamzito/ kupata mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au vifaa vyovyote vya simu katika mazingira ya shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Ambatanisha na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.(Picha passport moja kwa kila mmoja)

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

..................................................................

DAFROSA BERNARD MWAMPONDELE.

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KAZIMA
TABORA

**SHULE YA SEKONDARI YA KAZIMA**

## A. FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI…………………………………………………..
2. TAREHE YA KUZALIWA………………………………………………..
3. MZAZI / MLEZI ……………………………………………….................
4. UHUSIANO NA MLEZI ………………………………………………....
5. MAHALI UNAPOISHI MZAZI / MLEZI,
   MKOA……………………………………………........
6. WILAYA ………………………………………………...
7. MTAA/KIJIJI…………………………………………
8. MAWASILIANO YA MZAZI/MLEZI………………………………………..
9. KABILA ………………………………………………..
10. KAZI YA MZAZI/ MLEZI ………………………………………………..
11. WAZAZI WAKO HAI AU WAMEFARIKI WEKA ALAMA YA ( √ )
    - BABA (AMEFARIKI) ( ) BABA YUPO HAI ( )
    - MAMA( AMEFARIKI) ( ) MAMA YUPO HAI ( )
12. NDUGU WENGINE WA KARIBU NA MZAZI / MLEZI AMBAO WANAWEZA KUTUMIKA KAMA WALEZI WA WANAFUNZI KAMA MZAZI / MLEZI HUSIKA HAYUPO

1……………………………..…..………MAHALI …..……..………… SIMU…………….

2……………………………..…..………MAHALI ………...………… SIMU…………….

3……………………….……..….…….MAHALI ………....………… SIMU……………

4……………………….……..…….….MAHALI …………………… SIMU……………

## B. MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi (jina la mwanafunzi) ……………………………………………….. nimesoma na kuelewa sheria, kanuni za taratibu za shule ya bweni, niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapo kuwa shule adhabu stahili ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

…………………………………....                                        ………………………………………

Saini ya Mwanafunzi                                        Saini ya Mkuu wa shule

**MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**KAZIMA SECONDARY SCHOOL**
**P.O.BOX 329**
**TABORA**
**………………………**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.**

**This form must be completed by a government medical officer**

**Students full name………………………………………………………………**

**Present age………………………………………………………………………**

**Blood test ………………………………………………………………………..**

**School examination …………………………………………………………….**

**T.B test……………………………………………………………….……….**

**Asthma ………………………………………………………………………….**

**Eye disorder ……………………………………………………………………**

**Nose disorder …………………………………………………………………..**

**Ear disorder ……………………………………………………………………**

**Skin disease …………………………………………………………………….**

**Anaemia………………………………………………………………………...**

**Chest ……………………………………………………………………………**

**Operations ………………………………………………….………………….**

**Serious accidents……………………………………………………………….**

**Any other infections disease….……………………………………………….**

**Pregnancy…………………………………………………………...……….**

**Additional information e.g., physical defects or impairment, chronic or family disease etc……………………………………………………………………………………………………**

**……………………………………………………………………………………….**

**I certify that I have personally examined Mr./miss ………and found him/her fit unit to purpose studies**

**Signature………………………………………….**

**Designation……………………………………..**

**(Official rubber stamps) …………………………**